*Kioo cha Lugha*
*Juzuu 1, Na. 2 (1995)*

# SANAA, UBUNIFU NA JAMII KATIKA NADHARIA YA FASIHI

F.E.M.K.Senkoro

## 1.0 Utangulizi: Usuli

Mjadala ulioanzishwa katika miaka ya 70 na wananadharia Waswahili wa mwanzo waliolishughulikia suala la maana ya neno *fasihi*, ulielekea kufifia katika miaka ya 80 na ya 90. Kufifia huku kuliwafanya wanafunzi na walimu wa fasihi ya Kiswahili wafikiri kuwa mjadala ulikwishafungwa. Uliwafanya wanafunzi na walimu wengi wa somo hilo ambao walikuwa wakiufuatilia kwa makini wafikirie kwamba mwisho wa mjadala huu ulishafikiwa, hasa historia yake ilipozingatiwa tangu enzi za, miongoni mwa wengineo, John Ramadhani, Tigiti Sengo, S.D. Kiango, Felician Nkwera na Peter Kirumbi ambako fasihi ilihusishwa zaidi na hisi pamoja na nguvu za Mungu ambaye alielezwa kuwa ndiye Msanii Mkuu; hadi kufikia enzi za Penina Muhando na Ndyanao Balisidya ambapo fasihi ilielezwa kuwa ni tawi la sanaa ambalo hutoa maudhui yake kwa kutumia lugha na kwa kupitia kwenye umbo dhahiri; na baadaye enzi za M.M.Mulokozi, K. Kahigi na labda F.E.M.K. Senkoro na wengineo ambako fasihi ilionekana kwamba zaidi ya kuwa ni tawi la sanaa, vilevile ni zao la mikono na akili ya mtu ambalo hutokana na mazingira ya hapa hapa duniani yaliyomzaa, yakamlea na kumkuza msanii anayeisana kazi hiyo ya fasihi. Hatimaye, katika kazi na nadharia azitoazo E. Kezilahabi, ilielezwa kuwa zaidi ya kwamba ni sanaa, fasihi ina matumizi makubwa ya ishara kiasi kwamba ishara ndiyo hasa hiyo fasihi.[1]

Katika makala hii tutajaribu kuonesha kuwa kwa hakika mjadala huu wa maana ya fasihi haujafikia mwisho wake kwani bado kuna maswali mengi tu ambayo hayajapatiwa majibu kikamilifu. Kimsingi, maswali haya bado yanaturejesha kule kule kwenye swali letu la awali: *Fasihi ni Nini?* Humu tutatumia mifano mingi kutoka kwa wahakiki na wananadharia Waswahili kwani lengo ni kujaribu kuona ni hatua gani ambayo wahakiki hao wameifikia kuhusu nadharia ya fasihi kwa jumla.

Ili kujaribu kulijibu swali hili, katika makala hii tutachunguza pia maana za sanaa na ubunifu, na hatimaye tutaangalia jinsi dhana hizi zinavyoeleza uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii. Katika kuuangalia uhusiano huu makala hii inahitimishwa kwa kuanzisha mjadala kuhusu ubunifu, itikadi na nafasi ya fasihi, hasa fasihi-andishi, katika jamii zenye kiwango cha chini sana cha maendeleo, Tanzania ikiwemo.

### 1.1 Fasihi Kama Sanaa

Maana ya fasihi ambayo hadi sasa imeelekea kukubaliwa na watu wengi katika mlolongo huo wa mijadala inaeleza kuwa *fasihi ni aina ya sanaa itoayo maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno yanayotamkwa au yaliyoandikwa*, kinyume na sanaa zinginezo kama vile za uchongaji wa vinyago ambao `lugha' yake kuu ni gogo la mti, au uchoraji wa picha ambao nyenzo yake ni ama karatasi au kitambaa na rangi mbalimbali. Katika maana hii tayari kuna utata. Kwanza, ni muhimu kujiuliza, iwapo fasihi ni aina ya sanaa, wananadharia Waswahili wameieleza sanaa kuwa ni nini?

### 1.1.1 Maana za Sanaa

#### 1.1.1.1 Sanaa na Mungu

Feliciana Nkwera na John Ramadhani walichukua mwelekeo wa Ki-Socrati na Ki-Plato wa kumwona Mungu kuwa ndiye Msanii Mkuu, na kwamba sanaa yoyote ile hutoka kwa Mungu huyo ambaye humjalia msanii ufunuo wa kuumba kazi nzuri ya kisanaa. Ndiyo sababu hata maana ya fasihi aitoayo Nkwera inaambatana na uungu huo anaposema:

> Fasihi ni sanaa ambayo huanzia kwa Muumba, humfikia mtu katika vipengele mbalimbali.... (ni) hekima ambayo mtu ameshirikishwa apate kumtambua muumba wake.[2]

John Ramadhani naye ni mfuasi wa fasili hii ya sanaa anaposema kuwa matengenezo ya sanaa huonekana kuwa ni shughuli ya kiungu, na kwamba shughuli hii humwiga Mungu ambaye ndiye msanii wa kwanza.[3]

Kwa hiyo basi, kwa maoni ya wananadharia hawa, sanaa huanzia kwa Mungu na kumfikia msanii kwa njia ya ufunuo; na hapo ndipo msanii huyo huitoa sanaa hiyo kwa jamii.

#### 1.1.1.2 Sanaa Kama Uzuri

Katika kitabu chao cha *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*, Muhando na Balisidya wanakwenda mbele zaidi kwa kuihusisha sanaa na mtu. Wao wanaielezea sanaa kuwa ni uzuri ujitokezao katika umbo dhahiri.[4] Katika maana hii kuna utata ambao umejitokeza. Utata huu unaonekana pia pale Penina O. Mlama katika makala yake ya "Sanaa za Maonyesho Katika Jamii ya Asili" anapoeleza maana ya sanaa kuwa ni uzuri katika umbo sanifu. Anasema:

> Sanaa ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililo-sanifiwa; umbo ambalo mtu hulitumia kueleza hisi zinazomgusa kwa kutoa kielelezo au vielelezo vyenye dhana maalumu.[5]

Mlama ameendelea kwa kuiainisha sanaa katika mafungu makuu matatu: Kwanza kuna kundi la sanaa ambazo uzuri wake uko kwenye **umbo la kudumu**. Hizi ni "Sanaa za kuonyesha", kwa mfano utarizi, vinyago, picha za kuchorwa, n.k. Kundi la pili ni la **Sanaa za ghibu**. Mlama anaeleza kuwa sanaa za aina hii hazina uzuri ujitokezao katika umbo linaloonekana kwa macho au kushikika, bali hujitokeza katika umbo ambalo linagusika kihisia. Ametaja ushairi, uimbaji, na upigaji muziki kuwa ndizo aina za sanaa hii. Mlama anahitimisha kwamba kusikika ndiyo sifa kubwa ya sanaa hizi. Kundi la tatu na la mwisho ambalo Mlama ameliainisha ni lile la **Sanaa za vitendo**, yaani sanaa za maonyesho, ambazo uzuri wake hung'amuliwa pale zinapoonyeshwa mbele ya hadhira.

Wakati ambapo aina hizi kuu ambazo ameziorodhesha Mlama zinatufafanulia zaidi maana ya sanaa, bado kuna maswali kadhaa yanayohitaji kujibiwa kuhusu maana hii. Mathalani, ni vigumu kufahamu kuwa tanzu zingine za fasihi kama vile riwaya na hadithi fupi zinajitokeza wapi katika aina hizo tatu.

### 1.1.3 Sanaa Kama Mwigo Uvutao Hisia

Maana alizozitoa F.E.M.K. Senkoro zina matatizo yake vile vilevile. Mathalani, katika *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*[6] anasema:

> Sanaa ni uoanishaji mzuri wa fani na maudhui katika kazi ya mwigo aifanyayo mtu. Tanzu za sanaa hukua, hubadilika, na hata wakati mwingine hupigwa

vikumbo na nguvu za kijamii zikabaki kuwa historia katika kumbukumbu za nyaraka za kale.[7]

Katika *Fasihi na Jamii* Senkoro ameieleza maana ya sanaa kwa kirefu zaidi kwa kusema:

> Sanaa ni kazi ya binadamu yenye mwigo wa uyakini uliofungamana na wakati, mazingira, na mfumo wa jamii inayohusika. Sanaa ni kazi ya mikono na akili ya mtu, nayo aghalabu ina umbo dhahiri lenye maana/dhana maalumu.[8]

Kabla ya kuzijadili kwa undani maana hizi zilizotolewa kuhusu sanaa, tutoe dondoo la mwisho ambalo linatoka kwa Benedict Syambo na Alamin Mazrui katika kitabu chao cha *Uchambuzi wa Fasihi*.[9] Wao wanasema:

> Sanaa ni njia moja ya kumweleza mtu kitu fulani pamoja na kumfanya awe na hisia fulani juu ya kitu hicho. Kwa mfano, muziki ni sanaa, na kutegemea mdundo wake, unaweza kutufanya tuhisi furaha au huzuni, tuchangamke au tusikitike.[10]

Kwa kiasi kikubwa, maana wazitoazo Senkoro na Syambo/Mazrui ni za jumla mno. Mathalani, iwapo sanaa ni njia tu mojawapo ya kumweleza mtu kitu fulani na kumfanya awe na hisia fulani juu ya kitu hicho, je, hadhira inapohutubiwa na mwanasiasa na kuhamasika kwa hisi za ama furaha au chuki, hotuba hiyo ni kazi ya kisanaa?

Labda katika hatua hii tunaweza kuipanua kidogo maana ya sanaa na kutamka kuwa *sanaa ni ubunifu unaojitokeza katika aina aina za maumbo ya kiasilia, kiutumizi au kiumbuji*. Wakati ambapo katika sanaa za asilia hakuna ubunifu wa kiurazini, kwa hiyo si lazima sanaa iwe kazi ya mikono na akili ya mtu kama alivyodai Senkoro; katika zile za kiutumizi na kiumbuji kuna ubunifu wa kiurazini. Labda tutoe maelezo zaidi kuhusu aina hizi za sanaa.

#### 1.1.3.1 Sanaa Asilia

Mtu anapotazama sega la nyuki na jinsi lilivyopangwa vizuri ni dhahiri kuwa hugundua usanii wa hali ya juu. Ijapokuwa kuna nadharia zinazoeleza kuhusu urazini wa nyuki katika ubunifu wa kutengeneza masega, tujuavyo ni kwamba pamoja na usanii wote unaojitokeza katika masega hayo, hakuna urazini wa kukaa na kupanga na kubuni. Utengenezaji wa masega ya nyuki ni sehemu tu ya matendo yasorazini sawa na vile jicho linavyofumba haraka linapoona mdudu au uchafu unaokaribia kuliingia bila ya mtu kujishauri kuwa alifumbe jicho hilo au la.

Katika kundi hili la sanaa asilia tunaweza pia kutaja maua yenye rangi mbalimbali za kuvutia, vipepeo ambao wana rangi na marembo ya ajabu sana, upinde wa mvua unaotoa rangi mzomzo zinazovuta hisia za mtazamaji, na rangi za mvuto usio na kifani, za mkia wa tausi dume. Hizi zote zina usanii ambao haukuamuliwa kiurazini bali ulitokea tu, na ndiyo maana tumeziita kuwa ni sanaa asilia.

#### 1.1.3.2 Sanaa Tumizi

Katika kundi hili mna kazi za sanaa ambazo madhumuni yake makubwa ni ya kiutumizi zaidi ya kuwa na mvuto wa kiufundi. Mara nyingi mtu huvutiwa na mkeka au kikapu kilichofumwa vizuri ijapokuwa kimsingi mtu huyo atanunua vitu hivyo ili avitumie kulalia/kukalia au kuendea sokoni. Mtu atavutiwa na kitanda kilichotengenezwa vizuri sana na seremala, na hata atakinunua, ijapokuwa ununuzi wake huo utakuwa umelenga kwenye kukilalia kitanda hicho na si kuukodolea macho tu uzuri wake utokanao na marembo aliyoyatia fundi seremala. Vivyo hivyo, watu hupendezewa na majengo yaliyojengwa kiufundi, lakini madhumuni ya majengo hayo ni ya

kiutumizi badala ya kuwa tu vivutio vya njaa za kiumbuji za wanaoyatazama na kuyastaajabia. Hii yote ni mifano ya sanaa tumizi.

### 1.1.3.3 Sanaa Umbuji

Sanaa umbuji hukusanya zile aina za sanaa ambazo Mlama ameziita kuwa ni za ghibu pamoja na zile za maonyesho. Kwa kawaida, ukiachilia mbali nyenzo na vikorombwezo vinavyoweza kutumiwa katika kuzitoa sanaa hizo, hizi ni sanaa ambazo hazishikiki. Ni sanaa za kifikra zaidi. Hizi ni sanaa zisizo na umbo la kuonekana, ukiachilia mbali viwakilisho vyake ambavyo mara nyingi ni maneno yanayotamkwa, kusomwa, au kuimbwa. Katika fungu hili basi, imo fasihi.

## 1.2 Tofauti ya Fasihi na Aina Zingine za Matumizi ya Maneno

Swali kubwa linalozuka hapa ni, je, tutatofautishaje kazi ya fasihi na mazungumzo au maandishi ya kawaida? Mathalani, hotuba nzuri ya kisiasa ambayo ndani yake mwanasiasa katumia mifano kochokocho, na mafumbo pamoja na nahau na misemo, itatofautishwaje na kazi ya fasihi? Si humu pia mwanasiasa huyo ameitumia lugha kisanaa katika kutoa maudhui yake?

Hili ni swali gumu, lakini labda tuwezalo kusema hapa ni kwamba zaidi ya kuwa fasihi ni *utoaji wa maudhui kisanaa kwa kutumia lugha ya maneno ya kutamkwa au kuandikwa*, viko vipengele kadhaa vinavyoibainisha kazi ya fasihi na mazungumzo au maandishi ya kawaida kama vile hotuba au taaluma zinginezo. Baadhi ya vipengele hivi ni:

- **Mandhari, wahusika, na matukio** ambayo kwa kawaida ni mandhari, wahusika na matukio ya kubuni ijapokuwa hapohapo huwakilisha hali halisi za maisha;

- Aina ya **hadhira** na **muktadha** ambamo hadhira hiyo imo;

- **Matazamio** ya hadhira hiyo; yaani yale mambo ambayo hadhira imekusudia na inategemea kuyapata katika kazi ya fasihi au habari inayohusika. Mathalani, hadhira ya mkutano wa kisiasa haitakuwa na matarajio ya kupata tamathali za semi kwa wingi sana kutoka katika hotuba ya mwanasiasa, wala hawatapima kufaulu au kushindwa kwa hotuba hiyo kwa kutumia **vipengele vya kisanaa** vinavyotumika kupima kufaulu au kutokufaulu kwa kazi ya fasihi.

Kwa hiyo basi, msanii wa fasihi huunganisha pamoja mandhari pamoja na wahusika na matukio ya kubuni ili kuleta kisa au visa fulani. Hadhira hujinasibisha na mandhari, wahusika na matukio hayo kutokana na uzoefu walioupitia katika maisha yao, na pia matazamio waliyo nayo. Lakini vile vile kujinasibisha huko kunaambatana na vionjo vya kiumbuji ambavyo hukidhiwa kwa kupitia katika vipengele mahsusi vya kisanaa ndani ya kazi ya fasihi. Humu ndimo ulimo uhusiano baina ya fasihi na jamii; uhusiano ambao tunauangalia kwa kirefu kidogo baadaye katika makala hii.

Katika miaka ya hivi karibuni wataalamu Waswahili wametoa maana zaidi za neno hili `fasihi'. Kati ya hao yumo Said A. Mohamed ambaye katika kitabu chake cha *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi* [11] ameorodhesha sifa kadhaa kuwa ndizo zinazoibainisha kazi ya fasihi.

Kwanza, Mohamed anasema kuwa fasihi ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha, tena yenye kuvutia sikio, macho, tafakuri na hisia; yaani ni kazi yenye kupendeza na kuburudisha. Kazi hii inatarajiwa kuibuka na upya wa aina fulani katika mpangilio wa aina fulani kiherufi, kimaneno na kisentensi; yaani ni kazi yenye muundo fulani. Mohamed anaendelea kusema kuwa kazi hii huwa inatungwa kutokana na fikra au hisi za mtunzi. Hisi na fikra hizi hutokana na jamii finyu au pana ya mtunzi (familia, kijiji, wilaya, jimbo/mkoa, nchi nzima au ulimwengu wote). Zaidi ya hivyo, mhakiki huyu anasema kuwa kazi ya fasihi huwa ina uwiano au mwala (upatanisho)

fulani, yaani uzani au vipimo mwafaka vya kimawazo, kimuundo na kilugha. Kazi ya fasihi huwa imebeba mawazo, fikra, falsafa na hisi za mtungaji katika mtazamo wake wa kibinafsi, kuziwasilisha kwa hadhira. Katika kuifafanua zaidi dhana hii ya fasihi, Mohamed anasema kuwa kazi ya fasihi inaweza kuhusiana na utamaduni, maisha, uchumi, siasa, dini, elimu, saikolojia na nafsi ya mtunzi mwenyewe na jinsi ayaonavyo mambo mbalimbali ya nje (mazingira yote ya nje: ardhi na anga na vyote vilivyomo juu na ndani yake) na mazingira ya ndani yanayohusiana na dini, imani, roho, miungu, mashetani na nguvu zote tusizoziona au zilizoko nje ya uwezo wa kawaida wa mtu.

Mohamed anagusia masuala muhimu ambayo hatuna budi kuyajadili hapa. Masuala ya kubuni, kuibuka na upya na kutunga kutokana na fikra na falsafa za mtunzi tutayapa nafasi mahsusi baadaye katika makala hii. Suala tunaloweza kulijadili hapa ni lile la sifa ya fasihi kuwa na lugha yenye kuvutia, kupendeza na kuburudisha. Suala hili linao utata wake. Kuvutia, kupendeza na kuburudisha hutegemea maudhui yanayoshughulikiwa na kazi fulani ya fasihi. Kazi za kitanzia haziwezi kuwa na lugha yenye kuburudisha, bali lugha na matukio yake yatasikitisha na hata kuogopesha. Huenda "lugha" aliyokuwa akiiongelea Mohamed hapa ni sawa na ile sifa aliyoitoa Mlama ya `uzuri ujitokezao." Huenda ni ile sifa ya kwamba, hata kama mtunzi wa kazi ya fasihi anashughulikia jambo la kusikitisha atatumia lugha ya kipicha, iliyopambwa na tamathali za semi na vipengele vingine vya kisanaa ambavyo hutoa *mvuto* wa kiumbuji. Vipengele hivyo ndivyo vinavyotofautisha kazi ya fasihi na mazungumzo/maandiko ya kawaida au hotuba za kisiasa, hata kama mazungumzo hayo au hotuba hizo zitakuwa zinahusu maudhui hayo hayo yanayoshughulikiwa na hiyo kazi ya fasihi.

## 2.0 Ubunifu, Fasihi na Jamii

Kwa vile neno ubunifu, kubuni na hata "ubunaji" limejitokeza mara nyingi katika baadhi kubwa ya maana za fasihi zilizotolewa na wananadharia wa Kiswahili, hasa wa hivi karibuni, katika sehemu hii tutajaribu kueleza nafasi ya dhana hii katika dunia ya fasihi na katika uhusiano baina ya fasihi na uhalisi wa maisha ya jamii.

Katika makala yake ya "Kuandika Hadithi za Kubuni," Muhammed Said Abdulla anaonyesha jinsi ambavyo mstari unaotenganisha kweli na uongo katika kubuni ni mwembamba mno, na hata wakati mwingine haupo. Anasema:

> Kuweza kuzua uwongo uliofanana na kweli ni kutunga au kubuni. Kubuni ni *kuumba* kiumbe kwa fikra na mawazo bila kukiunda hata kikawa kinashikika; bali ingawa kuumba huko ni kwa mawazo tu, kiumbe cha kubuni kina sifa zote za kiumbe cha kweli....Katika *dunia* hiyo, au ulimwengu huo, viumbe vyenye tabia namna kwa namna huumbwa, na mambo kadha wa kadha hutungwa yakaachwa kutukia humohumo katika *dunia* yake..Kuitoa kazi....hiyo mbele za watu - kazi iliyofanywa kwa mawazo na fikara tu, halikuingia jiwe wala udongo - ndiyo kazi ya kuisimulia au kazi ya kuandika.[12]

Naye Said A. Mohamed ameeleza maana ya ubunifu, japo yeye anauita *ubunaji*, kama ifuatavyo:

> Ni hali inayompa msanii kuja na muundo au umbo fulani kutokana na hisi au mawazo fulani, umbo ambalo kwa namna fulani lina upya wa kimawazo na kimuundo au wa utumizi wa maneno au upya wa zana yoyote ile inayotumika kuundia au kubunia sanaa fulani.[13]

Said A. Mohamed anakiri kuwa hakuna ubunifu ambao hautegemei mambo yaliyomo kwenye uzoefu wa mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii kwa kusema:

> Hakuna ubunaji ambao hautegemei mambo yamo (sic) kwenye uzoefu na tajiriba zetu au za jamii zetu. Ubunaji hautokani na hali tupu (ombwe), bali unatokana na hali halisi, hali ya mambo ambayo msanii ameyaona, ameyasikia, ameyanusa, ameyaonja, ameyahisi au ameyasoma pahala. Kwa kutumia kipewa chake cha kubuni msanii atayafinyanga upya mambo hayo ili kuunda umbo la kisanaa.[14]

Kinyume na hayo, kuna mikururo ya mawazo ambayo inajaribu kuitenga fasihi na jamii. Baadhi ya mikururo hiyo ni kama ule wa *Hemetiki* na *Finominolojia*. Kwa kifupi wafuasi wa Hemetiki na Finominolojia wanasisitiza kuwa fasihi ni kiumbe ambacho kinajitegemea, chenye uhai na undani wake chenyewe, uhai ambao hauhusiani na mazingira yaliyomzaa wala kumlea msanii.[15]

Athari za mawazo kama hayo zimeanza kujitokeza hata miongoni mwa wahakiki na wanafasihi wa Kiswahili. Mathalani, Benedict Syambo na Alamin Mazrui katika kitabu chao cha *Uchambuzi wa Fasihi*[16] wanasema haya yafuatayo miongoni mwa mengi mengineyo:

> Utungo wa fasihi pia unaweza kutazamwa kama dunia ya kubuni inayojitosheleza yenyewe bila ya kuhusishwa na jambo lolote jingine la dunia hii yetu....Katika kutafiti mahusiano ya utungo na nafsi yake basi, maswali yanayohusu mtunzi, jumuiya ambayo utungo huo umetokana nayo, hadhira iliyodhamiriwa, tungo nyingine za wakati huo, yote huwa si muhimu.[17]

Kwa maana nyingine, kwa wataalamu hawa, saa ya ukutani au ya mkononi ni chombo tu kinachojitegemea, chombo ambacho aghalabu ni cha mviringo, chenye vijisehemu 12 vilivyogawanywa sawasawa, na ambavyo huzungukiwa na mishale miwili iliyofungiwa katikati kabisa, mmoja ukiwa mrefu zaidi ya mwingine. Chombo hiki hakihusiani kabisa na kupita kwa wakati kunakoashiriwa na kutua kwa jua, kutoka kwa mwezi na nyota, na kuchomoza kwa jua.

Ni wazi kwamba baadhi ya kazi za fasihi huweza kuonekana kama kwamba zinatawaliwa na hiyo dunia ya kubuni ambayo inajitosheleza yenyewe bila kuhusishwa na jambo jingine la dunia yetu hii. Mathalani, dunia ya hadithi nyingi za mapokeo inaonyesha majoka ya vichwa vingi na mazimwi ambayo humeza watu. Madubwana haya huangamiza vijiji na jumuia mbalimbali, na ni pale tu anapojitokeza kijana kutoka mbali ambaye anapambana na viumbe hawa katili na kuwaangamiza ndipo wanapohurishwa wale wote waliokuwa wamemezwa na majitu hayo. Hatimaye, katika dunia hii hii ya kubuni, vijana hao wanaopambana na majoka na mazimwi hutawazwa kuwa wafalme au viongozi wa wale waliowahurisha.

Msomaji au msikilizaji wa hadithi kama hizo huweza kuiona dunia hiyo kuwa ni ya peke yake, inayojitosheleza kwa kila hali bila kuitegemea dunia yetu hii. Kwani, katika uhalisi wa dunia yetu tuliyoizoea, haiwezekani liwepo joka lenye vichwa saba au sabini; wala haiwezekani kisayansi kuwa watu wamezwe na joka, wabaki mumo humo kwa siku kadhaa bila kukosa hewa wala kusagwasagwa na kufa tumboni mwa hilo joka. Vile vile, haiwezekani kijana mmoja apigane na joka la vichwa sabini na alishinde. Haya yote, na mengine ya namna hii, hayako katika dunia yetu tuliyoizoea.

Lakini vile vile ni vizuri kukumbuka kuwa **fasihi si uhalisi, wala si ukweli, bali ni mwigo wa ukweli na wa uhalisi**. Mwigo huu ndicho kipengele muhimu ambacho kinaipa kazi ya fasihi sifa ya ubunifu. Wakati ambapo hadithi hizo za madubwana, pamoja na zile za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Kufikirika* huweza kuonekana kuwa ni za kubunibuni tu

zilizojazana uongo kwani zinaeleza mambo yasiyowezekana kutokea katika dunia yetu hii, tukizingatia sifa ya mwigo tunaziangalia kazi hizo za fasihi kwa jicho lingine kabisa. Miongoni mwa vipengele ambavyo husaidia sana katika kujenga huo mwigo, vipo vipengele vinne vya fani na maudhui ambavyo ni muhimu sana. Hivyo ni: **Taswira, Ishara, Sitiari, na Falsafa**.

Tunapozitazama hadithi hizo za madubwana na hizo za Shaaban Robert kitaswira, kiishara, kisitiari na kifalsafa tunagundua kuwa hizi ni kazi za fasihi ambazo ubunifu wake unao uhusiano wa moja kwa moja na dunia yetu hii. Hii inamaanisha kuwa
kiungo baina ya hiyo dunia yetu tuliyoizoea na ile ya kubuni ambayo Syambo na Mazrui wameitaja, kiko katika fasili itokanayo na mbinu za kifasihi za fani na maudhui, hasa hizo nne tulizozitaja.

Labda, katika hatua hii tunaweza kutoa maana ya awali kabisa ya sifa hii ya ubunifu kuwa ni ule *uwezo wa kukifanya kitu au jambo kuwa na sura ya kuwezekana kuwapo hata kama hakuna uwezekano wa kuwapo kwa kitu au jambo hilo kwa hali hiyo.*
Ijapokuwa inawezekana kuuchukulia uhusiano huu kuwa sawa na ule wa kuku na yai, lakini haiyumkiniki mwanafasihi atunge au abuni kazi fulani ya fasihi halafu ndipo ajaribu kuona ina uhusiano gani na jamii. Ubunifu hutokana na uhalisi; bila kuwapo kwa uhalisi wa mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii hakuna ubunifu. Ndiyo sababu tunaweza kusema kuwa *ubunifu ni uwezo wa kuunda dunia mpya kutokana na dunia tuliyomo, ni uwezo wa kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo.*

## 2.1 Ubunifu Katika Fasihi ya Kihistoria

Iwapo basi maana ya ubunifu ni hiyo tuliyojaribu kuitoa hapo juu, ubunifu huo utakuwa na nafasi gani katika kazi za fasihi ambazo misingi yake ni ya kihistoria? Mathalani, wote tunaelewa kwamba Kinjeketile, Sundiata, Dedan Kimathi, na Fumo Liyongo ni mashujaa waliokwisha kuishi katika uhalisi wa historia ya Afrika; ni mashujaa ambao hata mashuleni hutajwa kwenye mihutasari ya somo la Historia. Sasa je, wanafasihi wanapoamua kuandika tamthilia, riwaya au mashairi ya kihistoria kuhusu mashujaa hao, na iwapo ubunifu ni sifa mojawapo ya kuzingatiwa wakati wa kutoa maana ya fasihi, sifa hiyo itakuwa na nafasi gani katika kazi hizo za kihistoria?

Hapa ndipo ile maana yetu ya kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo hujitokeza. Ijapokuwa wahusika hao waliishi kiuhalisi katika historia, lakini hawa wa kazi za fasihi wamepewa mawanda mapana zaidi ya kawaida tunayoijua kuwahusu wao. Mathalani, sifa ya Kinjeketile kuzama na kukaa mtoni kwa siku saba kama inavyojitokeza katika tamthilia ya E.N. Hussein, *Kinjeketile*, ni sifa ya kifasihi na wala si ya kihistoria. Tujuavyo, mtu hawezi kukaa ndani ya maji kwa zaidi ya dakika moja hivi bila kuibuka ili apate hewa, labda kama amebeba tenki la oksijeni, jambo ambalo Kinjeketile hakufanya. Lakini ulimwengu wa ubunifu unamruhusu Kinjeketile akae humo kwa siku kadhaa, na sisi kama hadhira hatutakiwi tuulize kuhusu uhalali wa dai hili kwani ubunifu wa ulimwengu wa kifasihi na urazini wetu wa kiumbuji unaruhusu mambo kama haya. Kwa hiyo basi, itakuwa ni kushindwa kuwa na jicho la kifasihi iwapo tutahitimisha kuwa matukio kama haya yanadhihirisha kuwa fasihi ni uongo. Ni katika "uongo" kama huo wa kubuni ndimo mlimojificha ukweli wa kifasihi kuhusu maisha. Huu ndio ule uwezo aliouongelea M.S. Abdulla wa kuzua uongo uliofanana na kweli.

Mfano mwingine ni wa Fumo Liyongo ambaye alipewa nguvu za ajabu zilizomfanya aogopwe katika nchi nzima. Hata mwili wake uliweza kukaa siku kadhaa kisimani ukiwa ameshikilia upinde na mishale bila kujulikana kuwa mwenyewe alikwishakufa siku tatu zilizopita. Hadhira ya Waswahili ambamo habari za Fumo Liyongo zilitambwa kwenye tenzi na mashairi, huwa tayari ina mvuto wa kiumbuji ambao hauwaruhusu kuuliza uhalali wa madai hayo. Kwa hiyo basi, mambo yote yale ambayo yanatufanya sisi kama hadhira kuweza kuwatofautisha mashujaa hawa wa kihistoria na mashujaa hawa hawa wa kifasihi ndiyo yanayounda hiyo sifa ya ubunifu.

Vile vile wahusika hawa watakuwa wamezungukwa na wahusika wengine ambao si lazima wawe wameishi katika historia halisi tunayoifahamu, na mambo wanayoyawaza na kuyasema si lazima yawe yaleyale ambayo waliyawaza na kuyasema katika maisha halisi. Ndiyo maana ni muhimu kusisitiza sifa ya **mwigo** ambayo inaifanya kazi ya fasihi iweze kuvuka mipaka ya ukweli na uhalisi, na kuwa na ukweli au uhalisi zaidi ya ukweli au uhalisi wenyewe.

Katika mwigo huo wa ubunifu kuna kificho kinachoipa hadhira changamoto ya kutafuta hicho kilichofichwa. Kwa hakika, mojawapo ya sifa zinazoifanya kazi ya fasihi iwe nzuri ni huo mficho wenye kutoa chemshabongo. Iwapo kazi ya fasihi itaeleza mambo moja kwa moja bila huo mficho, kazi hiyo itakuwa na uchapwa ambao hautaitofautisha na mazungumzo au maandiko ya kawaida. Nadhani ndiyo maana tunapoilinganisha kazi ya *Lina Ubani* ya Penina Muhando na ile ya E.Hussein ya *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*, ijapokuwa zote mbili zinashughulikia maudhui karibu sawa, hadhira tunaona umuhimu zaidi wa sisi kumpa Hussein mji kuliko kumpa Muhando mji mwishoni mwa kazi zao kwa sababu Hussein katumia sifa hiyo ya mficho zaidi ya Muhando. Wakati ambapo ni rahisi kuwahusisha wahusika/matukio katika *Lina Ubani* na wahusika na matukio halisi ya Tanzania ya enzi za vita na Iddi Amin, si rahisi kuwahusisha wahusika na matukio ya *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* na wahusika na matukio mahsusi. Ugumu au urahisi wa uhusishwaji wa wahusika na matukio halisi katika kazi ya fasihi ndio unaoonyesha kufaulu au kushindwa kwa kipengele cha ubunifu katika kazi hiyo. Kwa maneno mengine, Muhando kaumba dunia inayokaribiana mno na ile tuliyoizoea kwa hiyo ikawa tamthilia yake ni kitendawili rahisi kukitegua, wakati ambapo Hussein kaumba dunia mpya kutokana na hii tuionayo kila siku, na kazi yake imekuwa ni kitendawili kigumu chenye kuhitaji mji.

## 3.0 Ubunifu na Nafasi ya Fasihi Katika Uhalisi wa Jamii: Mjadala

Frederick Engels aliwahi kuihusisha fasihi na uhalisi wa maisha wakati alipoelezea maana ya uhalisia (*realism*) kwa kusema kuwa zaidi ya kueleza jambo katika undani na ukweli wake, ni ***usawirishaji wa kikwelikweli wa wahusika mahsusi katika mazingira mahsusi.***

Naye V.I. Lenin ambaye alikuja baada ya Engels alionya katika makala yake ya "Party Organization and Party Literature", kuwa tusisisitize mno kuhusu utabaka wa kazi ya fasihi tukasahau kuwa katika uwanja huu nafasi kubwa haina budi kutolewa kwa ubunifu wa mtu binafsi, fikra zake na hata undotondoto au fantasia kwenye fani na maudhui ya kazi anayoisana.[18]

Kwa mtazamo huo basi, fasihi haiwezi kutawaliwa na masuala ya kiitikadi kwani si chombo cha kiitikadi tu bali ni kazi ya kubuni ambayo inatazamiwa kuzishibisha njaa za kiujumi za hadhira inayohusika. Na hili ndilo suala letu la mwisho katika mjadala huu.

Katika miaka ya 1970 na 80 miongoni mwa mengi ambayo Senkoro aliyasema kuhusu kazi za E. Kezilahabi, alimshambulia kuwa kazi zake zimejitenga mno na jamii.[19] Leo hii ni vigumu kuamini kuwa kuna kazi ya fasihi ambayo inaweza kujitenga na jamii kwani hata tendo la kujaribu kujitenga na jamii lenyewe ni la kijamii. Mawazo ya msanii ambayo yanafikia hatua hiyo ya kujaribu kujitenga na jamii yenyewe huwa yamefinyangwa na hiyo jamii. Kwa hiyo basi, hata kama ingekuwa kweli kuwa falsafa zinazomwongoza Kezilahabi katika uandishi wake zimejitenga mno na jamii, jambo ambalo hata hivyo linahitaji utafiti na data nyingi kabla ya kutolewa kauli ya mwisho kama hiyo, ni wazi kwamba Kezilahabi na mawazo na falsafa yake *ni mazao ya jamii*, nayo yanatokana na uzoefu wake wa kukulia Ukereweni na pia sehemu mbalimbali Tanzania na duniani. Hata pale ambapo inaelekea kuwa Kezilahabi kaamua kuziinua kazi zake za fasihi kifalsafa kiasi ambacho hazieleweki haraka kama itokeavyo katika *Nagona*, *Mzingile* na baadhi ya mashairi yake, hili si tendo la kujitenga na jamii, bali ni matokeo ya hali fulanifulani katika uzoefu wa Kezilahabi tangu malezi aliyoyapata, elimu katika seminari, shule

na vyuo vingine, na kadhalika. Haya yote ni mambo ya kijamii ambayo yameifinyanga sanaa aitoayo Kezilahabi.

Mwanzoni tulisema kuwa tutalishughulikia suala alilolieleza Said Ahmed Muhammed, la mwanafasihi "kuibuka na upya wa aina fulani" hasa kwa vile kazi ya fasihi inatungwa kutokana na fikra au hisi za mtunzi. Kutokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi huchota kutoka katika uzoefu na mazingira yaliyomzaa, kumlea na kumkuza msanii, ni vigumu kuona kazi ya fasihi ikiibuka na upya wa kimaudhui. Sana sana kazi hiyo huweza kuibuka na upya wa kifani, upya ambao hata hivyo, misingi yake itakuwa katika jamii vilevile. Kwa hakika, madhumuni ya fasihi si kuzua au kuibusha maudhui mapya, kwani fasihi haina uwezo huo. Fasihi husubiri "maudhui" hayo yawemo katika usuli wa kijamii ndipo iyasawiri. Fasihi ni sawa na mtu ambaye hana uwezo wa kuleta mvua, bali husubiri hadi aone dalili za mvua ndipo hutabiri kuhusu uzito wa mawingu yatakayokunya mvua kubwa; na mvua hiyo ikinyesha haitasemekana kuwa mtu huyo ameifanya inyeshe. Vivyo hivyo, fasihi haileti mapinduzi, bali huyasawiri hayo mapinduzi pale yanapotokea.

Kwa hiyo basi, pale ambapo fasihi imebeba mawazo, fikra, falsafa na hisia za mtungaji kama aelezavyo Said Ahmed Muhammed, na pia fasihi hiyo inapohusiana na utamaduni, maisha, uchumi, siasa, dini, elimu, saikolojia na nafsi ya mtunzi mwenyewe na jinsi ayaonavyo mambo mbalimbali ya nje na mazingira ya ndani; yote hayo hayatakuwa ya kubuni bali yatatokana na maisha halisi ya jamii. Kwa maneno mengine, kama tunakubaliana kuwa ubunifu ni uwezo wa kuunda dunia mpya kutokana na dunia tuliyomo, na uwezo wa kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo, basi ni dhahiri kuwa **kimsingi** hakuna ubunifu wowote katika kazi ya fasihi kwani huunda tu dunia kutokana na ile iliyopo tayari, na huanzisha kitu kutokana na kile ambacho tayari kipo. Hakuna ubunifu kwa sababu, kama asemavyo Kezilahabi:

> Katika kutengeneza (kuumba) binadamu anajiumba mwenyewe; anakuwa kama alivyo na wakati huo huo anaongozwa polepole pale ukweli unapojidhihirisha wenyewe, japo penye hatari.[20]

Kwa maneno mengine, mwanafasihi huiigiza jamii yake na hujiigiza mwenyewe wakati wa kusawiri hali za kijamii. Fasihi haiundi na wala haina uwezo wa kuunda hali hizo. Haya ni dhahiri hasa tukizingatia fasihi-andishi katika jamii masikini kama Tanzania. Asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania wanaishi vijijini ambako hali zao ni duni mno kiasi cha kushindwa kujikimu kwa mahitaji ya lazima kama chakula, nyumba, na nguo, ukiachilia mbali masuala ya uduni wa elimu, afya, na huduma zingine za kijamii. Ni vigumu kuona jinsi ambavyo ndoto za wengi wetu kuhusu uwezo wa fasihi wa kuleta mapinduzi huweza kutimia. Ndoto hizi zilijazana hasa katika miaka ya sabini ambako tuliongelea kuhusu "fasihi na mapinduzi katika jamii." Fasihi, hasa fasihi andishi, haiwezi kuleta mapinduzi katika hali za sasa za nchi masikini. Na katika suala hili hakuna utata wa yai na kuku. Ni pale tu umasikini utakapofutwa ili kumwezesha Mtanzania wa kawaida kujipatia mahitaji yote ya lazima, ndipo ambapo Mtanzania huyo ataweza kujenga utamaduni wa kiburdani wa usomaji unaohitajika. Ni pale tu ambapo Mtanzania hatajikuta katika mtihani mkubwa wa kuchagua baina ya kununua chakula au kitabu, ndipo atakapoipata fursa ya kimaendeleo ya kununua na kusoma vitabu. Kwa sasa hivi kukaa na kutazamia kuwa Mtanzania wa kawaida atanunua kitabu, atakisoma na kujipatia maarifa ya kuyageuza na kuyaboresha maisha yake ni ndoto ya mchana.

Vilevile, si rahisi kutegemea kuwa iwapo Mtanzania huyo hana uwezo na hata wakati mwingine hajui kusoma na kuandika, basi silaha yake kuu itakuwa ni fasihi simulizi. Kinyume na vile ambavyo imekuwa ikisifiwa mno, fasihi haina uwezo wa kuwa silaha ya mtu masikini. Sana sana mtu huyo anaweza kuitumia kama mdundiko wa kujistarehesha na kujisahaulishia matatizo yake ambayo mara hiyo humrejelea uso kwa uso agunduapo kuwa mdundiko huo umempeleka mbali mno na nyumbani, na pale arudipo katika uhalisi wa umasikini wake. Wala si rahisi kutazamia

kuwa mtu huyo masikini ataweza kuuamsha na kuugeuza moyo wa tajiri kwa kutumia fasihi simulizi. Hilo nalo litakuwa ni wazo la kiutopia.

Kwa hiyo, tunaweza kujiuliza swali la mwisho: *Je, inawezekana kuwa labda lengo kuu la fasihi ni kuburudisha tu na kumsahaulisha mtu matatizo yanayomkabili?*

## Tanibihi

1 Kwa maelezo zaidi kuhusu mawazo ya wahakiki hawa tazama, miongoni mwa kazi zinginezo, John Ramadhani, "Fasihi ya Kiswahili," katika *Mulika*, Na. 2 (1971), kur.6-11; T.S.Y.Sengo na S.D. Kiango, *Hisi Zetu: 1* (Dar es Salaam: Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, 1974); *Hisi Zetu: 2* (Dar es Salaam: Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, 1975), na *Hisi Zetu : 1 & 2* (Dar es Salaam: Longmans, 1974); Felician Nkwera, "Fasihi", katika J.P. Mbonde, Mhariri, *Uandishi wa Tanzania: Insha* (Nairobi/Kampala/Dar es Salaam: east african Literature Bureau, 1976); Peter Kirumbi, *Misingi ya Fasihi Simulizi* (Nairobi: Foundation Books, 1976); Penina Mhando na Ndyanao Balisidya, *Fasihi na Sanaa za Maonyesho* (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1976); Penina Muhando, katika Omari, C.K. na M. Mvungi, Wah., *Urithi wa Utamaduni Wetu*, (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House,1981); M.M. Mulokozi na K.K.Kahigi, *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1982); F.E.M.K. Senkoro, *Fasihi* (Dar es Salaam: Press and Publicity Centre, 1984), *Fasihi na Jamii* (Dar es Salaam: Press and Publicity Centre, 1987), *Ushairi:Nadharia na Tahakiki* (Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press, 1988).

2 Tazama Nkwera, Felician, "Fasihi", katika J.P.Mbonde, Mh., *Uandishi wa Tanzania: Insha* (Nairobi/Kampala/Dar es Salaam: East African Literature Bureau, 19976), uk. 62.

3 Ameyasema haya katika insha yake ya "Fasihi ya Kiswahili," katika *Mulika*, 2 (1971), kur. 6-11.

4(Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1976)

5 Kutoka katika Omari, C.K. na M. Mvungi, Wah., *Urithi wa Utamaduni Wetu*, (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1981), uk. 150.

6 (Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press, 1988)

7 k.h.j., Uk. 7.

8 Katika F.E.M.K. Senkoro, *Fasihi na Jamii* (Dar es Salaam: Press and Publicity Centre, 1987), uk.14.

9 (Nairobi: East African Educational Publishers, 1992)

10 Syambo, Benedict na Alamin Mazrui, k.h.j., uk. 1.

11 (Nairobi: Evans, 1990)

12 Katika Mbonde, J.M., Mh., *Uandishi wa Tanzania: Insha*, (Nairobi/Kampala/Dar es Salaam: East African Literature Bureau, 1976), uk. 101.

13 k.h.j., uk. 3.

14 k.h.j.

15 Kwa mjadala kuhusiana na mitazamo hii angalia makala ya Senkoro, F.E.M.K., "The Abstract and Social Bases of Literary and Artistic Styles," Makala iliyotolewa katika semina ya Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 1990. Inapatikana Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hapa tunaweza kutoa mifano michache tu ya namna mjadala ulivyoendelea kwa mtazamo wa Kihemetiki na Kifinominolojia. Mathalani, Edmund Husserl alisisitiza kuwa utafiti wa njia ya kuona ukweli wa mambo, hatimaye huikataa hali iliyodai kuwa vitu vipo huria nje ya mawazo ya mtu. Kutokana na mtazamo huu basi, **vitu havipo vyenyewe bali vipo kwa kuwa katika fahamu za mtu**. Kwa hiyo basi, ufahamu hujengwa katika fahamu ya mtu juu ya kitu. Ili kujenga "hakika" ya finomena, hatuna budi kuufinya ulimwengu wa nje na kubaki na vitu vilivyomo ndani ya fikra zetu tu. Finominolojia, basi, ni sayansi ya vitu halisi ndani ya fikra. Kutokana na mitazamo kama huu ndipo walipozuka Wanaumundo ambao wanadai kuwa matini ya kifasihi inafanya mfumo unaojitegemea nje ya mazingira halisi ya mwanafasihi. Kwa hiyo wanasema kuwa si vizuri kutoka nje ya matini hiyo. Hata hivyo, Heidegger, mwanafunzi wa Husserl alimsahihisha mwalimu wake kwa kusisitiza kuwa mtu yumo ndani ya hali halisi, na mtu ni mdhibiti wa maisha. Mtu huyo hajakamilika, na yumo katika mwendo wa kukamilika kufuatilia historia na wakati.

Msomaji mwenye kutaka kufahamu zaidi kuhusu masuala haya anashauriwa pia kumsoma V. Shklovsky (1917), katika "Art as Device" ambako anasema kuwa sanaa hufanya kitu kiwe kigeni; nayo ni njia ya kupata usanifu (ubaya au uzuri) wa kitu ijapokuwa kitu chenyewe si muhimu. Hili lilielekea kuungwa mkono na wataalamu wa baadaye wa fasihi na isimu. Mathalani, Ferdinand de Saussure, katika *Course in General Linguistics* (London: Peter Owen, 1974)anasema kuwa lugha hueleza dhana ya kitu, haielezi kitu chenyewe; kwa hiyo lugha ni kielezeo na kitu ni kielezwa. Maana ya kitu basi, inakuwa ndani ya kielezeo, na kielezeo hiki kinaposhirikiana na vielezeo vingine hujenga ulimwengu unaojitegemea. Kwa hiyo lugha ni chombo kinachojitegemea. Ndiyo maana wanaumundo nao wanadai kuwa maana ya kitu iko katika dhana. Wanafuatia nyayo za Lacan ambaye anasema, "Siwezi `kumaanika' na `kuwa' kwa wakati huo huo mmoja", msemo ambao huweza kuhusishwa na ule wa kiingereza kuwa huwezi kuila keki yako na wakati huo huo ukabaki nayo.

16 (Nairobi: East African Educational Publishers, 1992)

17 k.h.j., uk. xiii.

18 Kwa maneno yake mwenyewe alisema:

> Literature is least of all subject to mechanical adjustment or levelling, to the rule of the majority over the minority. There is no question, either, that in this field greater scope must undoubtedly be allowed for personal initiative, individual inclination, thought and fantasy, form and content."

19 Angalia, kwa mfano, "Sura ya Tatu: E.Kezilahabi: Dunia Uwanja wa Fujo" katika *Fasihi* (Dar es Salaam: Press and Publicity Centre, 1984) kur.81-91 na pia katika makala iliyotajwa hapo juu, na pia katika Sura ya 2 ya *Fasihi na Jamii* ambamo, miongoni mwa mengine mengi nilisema hivi:

> Katika..Dunia Uwanja wa Fujo...ijapokuwa mwandishi kwa kiasi fulani anagusia matatizo ya jamii ya Tanzania baada ya Azimio la Arusha, falsafa yake anayoihubiri kuhitimisha kazi yake hii ni

> kuwa maisha ni fujo na vurugu tupu....Kwa welekeo wa aina hii,
> Kezilahabi kazifanya riwaya zake zijitenge na jamii..
>
> (uk.29)

20 Kezilahabi, E. "Siasa, Tekinoojia na Ukuaji wa Fasihi ya Kiswahili," katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu 1 Na. 1 (1995), uk.59.